

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
Julai 2014
Saa: 2 ½



SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA ALLIANCE

MTIHANI WA MWIGO – 2014

Jumane 15 Julai, 2014 - 8.00 – 10.30 Asubuhi

Maagizo

1. *Jibu maswali manne pekee.*
2. *Swali la kwanza ni la lazima.*
3. *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Tamthilia, Hadithi Fupi, Ushairi, na Fasihi Simulizi.*
4. *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
5. *Karatasi hii ina kurasa 6 zilizopigwa chapa.*
6. *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*
7. *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

© 2014 Shule ya Upili ya Wasichana ya Alliance
Mtihani wa Mwigo - Fasihi

SEHEMU YA A: RIWAYA

Ken Walibora: Kidagaa Kimemwozea.

Lazima

- (1). "Ndugu usinifikirie mwendawazimu lakini uchanganuzi wangu unaniambia kuwa wewe si mtu wa kawaida."
- (a). Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- (b). Fafanua umuhimu wa msemaji kwa kurejelea riwaya nzima. (al. 6)
- (c). Eleza jinsi Mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea alivyosawiri maudhui ya mapuuza. (alama 10)

SEHEMU YA B: TAMTHILIA

Timothy Arege: Mstahiki Meya

Jibu swali la 2 au la 3

- (2). "Shinikizo lililokuwepo lingetuaa."
- (a). Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- (b). Fafanua tamathali ya usemi iliyojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
- (c). Eleza sifa zozote tatu za msemaji (alama 6)
- (d). Jadili shinikizo linalorejelewa katika dondoo hili (alama 8)
- (3). Anwani ya Mstahiki Meya ni ya kitashititi. Thibitisha. (alama 20)

© 2014 Shule ya Upili ya Wasichana ya Alliance
Mtihani wa Mwigo - Fasihi

SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

Ken Walibora na Said A. Mohamed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.

Jibu swali la 4 au la 5

- (4). “Wambie lilo la kweli, wasikutafute, oo ‘sitafute”
- (a). Yaweke maneno haya katika mkutadha wake. (alama 4)
- (b). Fafanua mbinu ya kisanaa inayodokezwa katika nukuu hii. (alama 2)
- (c). Jadili ‘ukweli’ unaorejelewa katika dondoo hili. (alama 14)
- (5). Kwa kurejelea diwani nzima, jadili jinsi ambavyo wanawake wanadunishwa. (alama 20)

SEHEMU YA D: USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

- (6). **Soma ushairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Wenzangu nisikizeni, kwa uchungu ninalia,
Nimefungwa kwa katani, siwezi kujifungua,
Muhibu wangu ni nani, ataye kuniokoa,
Ninamuomba Jalia, niepushe na shetani.

Ukimwona Sulemani, kiatu kajikwatua,
Na saaye mkononi, alamaye ni kofia,
Nilimwona Sulemani, hofu iliniingia,
Ninamuomba Jalia, niepushe na shetani.

*© 2014 Shule ya Upili ya Wasichana ya Alliance
Mtihani wa Mwigo - Fasihi*

Macho yake samahani, hayani meshanitia,
Mdomo wake jamani, pia unanivutia,
Mwenzenu ni matatani, kwa kweli kanivutia,
Ninamuomba Jalia, niepushe na shetani.

Babangu kule nyumbani, mbali kanifukuzia,
Kaniita hayawani, kwake guu sijetia,
Huruma nioneeni, natubu nimekosea,
Ninamuomba Jalia, niepushe na shetani.

Wasichana sikulini, dunia imechafuka,
Mtafungwa kwa katani, nanyi mtaghafilika,
Nikiwa na Sulemani, kabisa napotezeka,
Ninamuomba Jalia, niepushe na shetani.

- (a). Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)
- (b). Fafanua bahari katika shairi hili. (alama 6)
- (c). Andika ubeti wa tano katika lugha nathari. (alama 4)
- (d). Fafanua kwa kutoa mifano, mbinu **tatu** alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (alama 6)
- (e). Bainisha nafsineni na nafsinenewa katika shairi hili (alama 2)

(7). Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Jogoo la kwanza liliwika,
Tuliolala tukaamka,
Tulidhani kumepambazuka,
Kaniki nyongani,
Jembe libegani,
Panga mkononi,
Nimekwenda shambani,
Hakujacha.

3. Nje hakuna aliyetoka,
Hofu nyingi zikatighubika,
Vibandani tunatetemeka. Tukabaki
ndani,
Na nyingi huzuni,
Simanzi nyoyoni,
Roho mikononi
Hakujacha.

2. Kabla ya nje haujatoka,
Mvua mkubwa kaporomoka,
Radi na umeme kusikia,
Bundi akalia,
Akaashira,
Nuksi kutujiya,
Baa kuingia,
Hakujacha.

4. Bundi hataki kubanduka, yu
paani amejipachika,
Lalia kila dadika,
Mambo si salama,
Hakuna uzima,
Ila ni nakama,
Sote twayoyoma,
Hakujacha.

- (a). Nafsineni alalalamika kuhusu nini? (alama 2)
- (b). Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)
- (c). Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili. (alama 4)
- (d). Jadili sifa za utunzi alizotumia mshairi katika wa ubeti wa tatu. (al. 3)
- (e). Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alama 4)
- (f). Mishata ni nini? Toa mifano yoyote miwili inayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)
- (g). Fafanua maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika shairi. (alama 2)
 - (i). kaniki
 - (ii). nakama

8) SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

- (a). Eleza maana ya ngoma. (alama 2)
- (b). Fafanua sifa zozote tatu za ngoma. (alama 6)
- (c). Ngoma ina majukumu gani katika jamii. (alama 12)

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA

© 2014 Shule ya Upili ya Wasichana ya Alliance
Mtihani wa Mwigo - Fasihi